

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZAN
OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
SHULE YA SEKONDARI RUNDUGAI S.L.P. 78, HAI

TAREHE 15/12/2020

Kumb Na RSS/K I/2021

MZAZI WA

.....

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUNDUGAI WILAYA YA HAI MKOA
WA KILIMANJARO MWAKA 2021**

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Rundugai ipo umbali wa km 11 kusini mwa mji mkuu wa wilaya ya **Hai** yaani mji wa **Boma ng'ombe**. Pia shule ipo km 1 kutoka maduka ya Rundugai barabara iendayo kijiji cha chemka.

Shule itafunguliwa kwa mhula wa kwanza tarehe 11/01/2021 . Mzazi unatakiwa kumleta mwanao shuleni kuanzia tarehe iliyopangwa na mwisho wa kuripoti ni i wiki mbili baada yashule kufunguliwa (siku 14) vinginevyo nafasi yake atapangiwa mwanafunzi mwingine na mzazi utachukuliwa hatua kwa kutokumpeleka mwanao shule pasipo sababu zozote za msingi.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.1 SARE ZA SHULE

a) Wavulana

- ❖ Suruali mbili za rangi ya **kijani kibichi**(**namba one**) suruali iwe na marinda mawili kila upande wa mbele.(asishone modo upana inch 16,17na kuendelea)
- ❖ Mashati mawili meupe mikono mifupi
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili na siyo buti
- ❖ Soksi nyeusi
- ❖ Sweta rangi ya **kijani kibichi**.

b) Wasichana

- ❖ Sketi mbili za rangi ya **kijani kibichi** (**namba one**) iwe na marinda kati ya kumi hadi kumi na tano (vipimo visiwe chini ya tumbo)
- ❖ Blausi /mashati mawili meupe ya mikono mifupi
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vyenye kamba na visiwe na kisigino kirefu
- ❖ Soksi nyeupe
- ❖ Sweta rangi ya **kijani kibichi**
- ❖ Hijabu ifanane na sare ya shule.(wale tu wanaotumia vazi hilo kulingana na imani.)

NB:Angalia **kitambaa** kilichoambatishwa kama mfano wa sare ya shule itakiwayo.

c) **Sare ya michezo**

- ❖ wavulana bukta ni rangi ya bluu na Tishit rangi ya maruuni (damu ya mzee)
- ❖ Wasichana bukta ni rangi ya bluu na Tshit rangi ya maruuni (damu ya mzee)

Au Traki suti rangi ya bluu yenye mistari mweupe kwa wavulana na wasichana

1.2 Daftari ,kalamu,na mkebe wa hesabu,begi,dictionary,mathematical table, calculator

1.3 Chakula: Ni jukumu la mzazi na kwa kupitia kamati ya wazazi iliyopo shuleni,upo utaratibu uliopangwa katika kikao halali na kupewa kibali cha kusimamia jukumu hilo.

1.4 Sahani ya chakula na kijiko

1.5 Nauli ya kuja shule na kurudi nyumbani kwa wale wanaotumia usafiri

1.6 Matibabu

1.7 Mahitaji mengine ya kibinadamu kama pedi kwa wasichana

1.8 Kifaa cha maji (ndoo ndogo ya lita 10 atakuwa anakuja nayo na kurudi nayo)

1.9 Picha moja ya passport kwa ajili ya kuweka kwenye faili la kukmbukumbu shuleni.

1:10 Miti miwili ,mmoja mti wa **tunda** lolote (isipokuwa mti wa msambarau hautapokelewa) na mti wa pili ni mti unaostahimili ukame usipokuwa mjohoro) mwanao atatunza miti hii muda wote awapo shuleni.Hili ni utekelezaji wa agizo la ngazi za juu.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na **OFISI YA RAIS –TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.mwanao anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- a) Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo muhimu shuleni.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya masomo jioni (preparation uwapo nyumbani)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;na
- i) Kutunza mali za umma.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE


- a) Wizi.
- b) Uasherati na Ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungu, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana na kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/Kupata mimba.
- i) Kuoja au kuolewa.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na **simu** ya mkononi.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakatolewa na shule

5.0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII


M.D. MATEMBA
MKUU WA SHULE

HEADMISTRESS
MUNDUGAI SECONDARY SCHOOL
HAI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
SHULE YA SEKONDARI RUNDUGAI

FOMU YA AHADI

SEHEMU A: MWANAFUNZI KUKUBALI SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Jina la mwanafunzi.....

Tarehe ya kuzaliwa(AMBATISHA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA)

Namba ya mtihani shule alikotoka.....

Jina la mzazi/mlezi.....

Uhusiano (undugu) na mzazi /mlezi.....(baba,mama,kaka,mjomba n.k

Kazi ya mzazi /mlezi.....

Namba ya simu ya Mzazi /Mlezi.....

Mahali anapoishi:Kata.....

Mtaa/kijij.....

KIAPO CHA UTII

Miminimesoma na kuelewa maelekezo na taratibu zote zilizoko hapo juu ,nikiwa mwanafunzi wa shule ya sekondari **RUNDUGAI** nakubali kuwa umma wanchi hii ya Tanzania ndio ulionipa nafasi hii maalum ya masomo,ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi yangu katika maendeleo yake.

Niko tayari kufuata taratibu hizo na naahidi kwamba,nitajibidisha nikiwa hapa shule na hata nje ya shule,na kwamba ili kutimiza shabaha hiyo,ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa sitashiriki katika **migomo, fujo na makosa ya jinai** nitatii na kufuata sheria,kanuni na taratibu za shule, pamoja na maelekezo yote halali nitakayopewa na walimu na viongozi wengine wa shule Endapo nitakuwa na maoni/mapendekezo yoyote naahidi kuwa nitayafikisha kwa viongozi wa shule/walimu kwa kufuata utaratibu bila ya kuogopa chochote.

Saini ya mwanafunzi.....

Tarehe.....

UTHIBITISHO WA UONGOZI WA SHULE

Tamko hili limepokelewa shuleni na:

Mhusika (Jina)

Wadhifa.....

SainiTarehe.....

Mhuri wa shule.....

SEHEMU B

ORODHA YA NDUGU /JAMAA WA MWANAFUNZI

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi akitoa maelezo sahihi ya ndugu/jamaa zake watano,watakaokupa huduma mbalimbali na kumtembelea wakati wa masomo hapa shuleni n.k

s/no	JINA LA NDUGU/JAMAA	UHUSIANO	ANWANI YAKE	NAMBA YA SIMU
1				
2				
3				
4				
5				

Nathibitisha kuwa taarifa hii ni sahihi kadri ya ufahamu wangu.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

Sahihi ya Mwanafunzi.....

Tarehe.....

SEHEMU C

KWA MATUMIZI YA OFISI

Jina la MwanafunziAdm No.....

Amefika shuleni tarehe

Amepangwa asome kidato cha kwanza mkondo/mchepuo wa

Tarehe.....Saini na mhuri

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
SHULE YA SEKONDARI RUNDUGAI

FOMU YA AHADI

SEHEMU C: MZAZI/MLEZI KUKUBALI SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

MZAZI/MLEZI WA

Mimi (kamili)

Mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari **Rundugai** kidato cha kwanza mwaka 2020 nakiri kusoma kwa makini maelezo na maagizo na kukubali kuyatekeleza kikamilifu sheria ,kanuni na taratibu za shule hii pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Naahidi na kuhakikisha kuwa mwanafunzi huyu atapata hudumu zitakiwazo kama ilivyoainishwa kwenye fomu ikiwa ni sehemu ya majukumu yangu kama mzazi /mlezi.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

Mahali anapoishi:Kata.....

Mtaa/kijij.....

Namba ya simu.....

Tarehe.....

UTHIBITISHO WA MKUU WA SHULE (au niliyepewa madaraka ya mkuu wa shule)Nathibitisha maelezo ya Mzazi /Mlezi na kuyasimamia .

Jina la Mkuu wa shule

Sahihi.....

Tarehe.....

Muhuri.....

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

RUNDUGAI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 78 HAI

PASSPORT
SIZE

RE:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examineas to his/her
Physical and mental fitness for admission to school as a student.

Name **MATEMBA M.D** signatureDate.....

MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by the medical officer at

- 1. Eye sight.....
- 2. Hearing.....
- 3. Limbs.....
- 4. Pregnanacy.....
- 5. Asthma.....
- 6. Tuberculosis.....
- 7. Venereal diseases.....
- 8. Covid 19.....
- 9. Other serious diseases.....

- i.
- ii.
- iii.

GENERAL COMMENTS:

.....
.....

Name of the Doctorsignature.....

Station.....Designation.....

Date.....